


UKATILI WA KIJINSIA

Kabla ya kwenda kuangalia maana ya ukatili wa kijinsia. Embu kwanza tuangalie maana ya maneno yanayotumika.

Maneno kama vile **Jinsi** na **Jinsia**

JINSI

JINSI: Ni hali ya kuwa na maumbile ya kike au ya kiume kwa maana nyengine ni maumbile aliyozaliwa nayo mwanamke au mwanaume na hayawezi kubadilika.



JINSIA

Ni neno na pia ni dhana. Kama neno, hutumika kuelezea mahusiano yakijamii kati ya mwanamke na mwanaume. Kama dhana, neno jinsia hutumika kuelezea tofauti za kijamii baina ya wanawake na wanaume ambazo zinaonekana kupitia mgawanyo wa kazi, upatikanaji na udhibiti wa rasilimali, mitazamo, tabia, maadili na uwezo au muundo wa kaya.



MAANA YA UKATILI WA KIJINSIA

Ukatili wa kijinsia ni kitendo anachofanyiwa mtu yeyote mwanamke au mwanaume kwa lengo la kumdhuru au kuumumiza kisaikolojia, kimwili, kiafya, kingono na kiuchumi. Hata hivyo tafiti nyingi zimeonyesha kwamba wanawake ndiyo wahanga wakuu wa ukatili wa kijinsia.

AINA ZA UKATILI WA KIJINSIA

Ukatili wa kijinsia umegawanyika katika makundi mbalimbali. Mfano

- Ukatili wa kimwili,
- Ukatili wa kisaikolojia,
- Ukatili wa kingono,
- Ukatili wa kiuchumi,
- Ukatili wa kiafya,

Ukatili huu unaweza kutokea katika mazingira tofauti tofauti ya maisha ya binadamu

Mfano:

- Katika maeneo unayofanyia kazi zako ama biashara zako
- Majumbani tunamoishi na watu tunaishi nao na kuwaamini
- Kwenye jamii zetu na kwenye maeneo tunayotembelea
- kupitia mitandao ya kijamii

SABABU ZA UKATILI WA KIJINSIA

- Mifumo ya kijamii isiyozingatia usawa baina ya wanawake na wanaume.
- Wanawake kutokuwa na sauti na ushiriki kwenye vyombo vya maamuzi ndani ya jamii
- Mitazamo hasi ya wanajamii kuwaona wanawake ni daraja la chini kuliko wanaume
- Nadharia zisizosahihi kuhusu majukumu ya wanawake na wanaume kwenye jamii
- Mifumo dume kwenye jamii inayolinda maslahi ya wanaume
- Mila, desturi na Tamaduni zenye kuleta madhara.
- Umaskini.
- Ukimya wa jamii kukemea matendo ya ukatili wa kijinsia ikiwemo kuwapa kinga na kuwatetea watendaji wa ukatili huo.
- Uelewa mdogo wa wanajamii kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia
- Imani potofu.

MAKOSA YA UKATILI WA KIJINSIA

1. Vitisho na lugha ya kufedhehesha
2. Kubaka
3. Kumla mande(Kundi la wanaume kushirikiana kumuingilia kingono mwanamke au msichana kwa zamu bila ya ridhaa yake)
4. Kujaribu kubaka
5. Ukeketaji
6. Kupoka au kutorosha
7. Shambulio la aibu(matendo yote yanayolenga kumfedhehesha mtu na kumtia aibu)
8. Kunajisi mtu mwenye ulemavu wa akili
9. Kutumikisha watoto katika uasherati
10. Uwakala au ushawishi wa kufanya ukahaba/umalaya
11. Usafirishaji wa binaadamu
12. Kutelekeza na kuacha kuhudumia familia,
13. Udhalilishaji wa kingono maofisini
14. Udhalilishaji kwa njia ya mitandao

MADHARA YA UKATILI WA KIINSIA



- a) Vifo
- b) Ulemavu wa kudumu
- c) Umaskini
- d) Unyonge na kuishi kwa hofu
- e) Msongo wa mawazo na kukosa furaha ya maisha
- f) Kuongezeka kwa watoto waishio katika mazingira magumu.
- g) Kuongezeka kwa maambukizo ya ukimwi

NINI KIFANYIKE



Kutokukaa kimya pale tuonapo matukio ya ukatili wa kijinsia katika jamii zetu. Kila mtu ana wajibu wa kuhakikisha matukio ya ukatili yanatokomezwa katika jamii zetu. Binadamu wote ni sawa na wanatakiwa kuheshimiwa utu wao bila kujali rangi, jinsia, maumbile, utaifa, hadhi ya ukimbizi, hali ya uchumi wala hali ya elimu.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA MTU ALIE LAWITIWA AMA KUBAKWA



- Usioge wala usinawe
- Kama inawezekana usibadili nguo
- Ikibidi kubadili nguo Usifue nguo baada ya kitendo cha ubakaji ipeleke polisi hivohivo, ihifadhi katika mfuko wa kaki au gazeti.

⚠ Usitumie mfuko wa plastiki kwa kua hugaribu Ushahidi

- Usichane wala kuosha nywele ili kukwepa kuharibu ushahidi
- Iwapo utapata haja ndogo hifadhi kwenye chombo kisafi kasha peleka hospitali kwa uchunguzi zaidi.
- Nenda katoe taarifa polisi
- Wakabidhi polisi vitu vyovyote unavyohisi vitakavyo tumia au vitakavyosaidia katika kupata ushahidi
- Mtu aliebakwa au kulawitiwa anatakiwa kufika kituo cha afya au zahanati ndani ya masaa 72 baada ya tukio.

Hii husaidia kupata huduma ya afya pamoja na zingine za kuzuia maambukizi ya UKIMWI kama PEP na mimba zisizotaraiwa.

NAMBA ZA KUPIGA KURIPOTI UNYANYASAJI WA KIJINSIA

- 0800780100 --- WLAC
- 0800780070---WILDAF
- 116

Kwa msaada wa kisheria au maelekezo zaidi unaweza kuwasiliana na **DIGNITY Kwanza** kupitia namba zifuatazo

0788609094
0699533211



Kimetayarishwa na:

DIGNITY Kwanza - Community Solutions
Nyumba na. 13, mtaa wa Vinyaji, Karibu na barabara ya
Cocacola kutoka kituo cha Bajaj Osama
Mikocheni B, Dar es Salaam
S.L.P 33035 Dar es Salaam;

Simu +255 22 27 81 176; au +255 788 609 094
Barua pepe : info@dignitykwanza.org;
Tovuti : www.dignitykwanza.org



UKATILI WA KIJINSIA